



## International Ecumenical Peace Convocation

Kingston | Jamaica | 2011

### Maombi kutoka Karibien – Jumapili, 22 Mei 2011

Mungu wa amani, Muweza wa yote, Muumba, Mwokozi na Mponyaji wetu.  
Tunakuja mbele zako tukiomba huruma yako na msamaha wako.  
Tunakuomba utusaidie kuleta amani katika dunia hii.  
Mara nydingi tumeviruga jitihada na mipango ya kuleta amani, badala ya kuushinda ubaya kwa wema.  
Bwana bado tunataka kuipa amani nafasi katika dunia hii.  
Hatukuchukua hatua wema ulipokiukwa.  
Ee bwana tunaomba utusamehe.

#### **Bwana tunakuomba utupe amani.**

Bwana jinsi tunavyokuomba msamaha ndivyo pia tunavyokuomba amani.  
Tunakubali upya jukumu letu kama waleta amani na watetezi wa haki.  
Tunashukuru kwa mwongo wa kushida ukatili na kazi zake zote,  
hasa kwa kutuongezea ufahamu na hamu ya kujenga amani.  
Tunatambua bado tunayo kazi kubwa katika kudumisha amani ulimwenguni.

#### **Bwana tunakuomba utupe amani**

Bwana tunakuomba roho wako mtakatifu aelekeze mioyo na akili zetu katika kuleta amani na atusaidie sisi tuweze kuwa watetezi wa haki. "Wakati wa amani uwe sasa." Tusaidie tuweze kushirikiana nawe katika kujenga ulimwengu ambapo amani itakuwa tabia na asili yetu.  
Tujalie hekima, imani ya kuweza kutambua yote yaletayo amani na ujasiri wa kukuamini na kuheshimu.

#### **Bwana tunakuomba utupe amani.**

Mungu wa amani na uwezekano, twakuomba utufanye kuwa vyombo vyaa amani yako, wakati huu wa kongamano la amani la kimataifa la kiokumene na mahali pengine pote ili tuweze kutimiza mapenzi yako. Kwa jina la Mfalme wa amani, Yesu Kristo, Bwana na Mwokozi wetu.  
Amina